## 30.2 KISWAHILI (102)

### 30.2.1 Kiswahili Karatasi ya 1 (102/1)

**Swali La Kwanza**

Tahariri Kwa Gazeti La Raia

**a) Sura**

- Iwe na kichwa.
- Iwe na tarehe.
- Iwe na utangulizi.
- Iwe na mwili/maelezo kiaya.
- Yaweza kuwa na maoni au msimamo wa mhariri au msimamo wa gazeti.
- Iwe na hitimisho k.m. jina la mhariri na wadhifa wake.

**b) Maudhui: Kuendeleza Msichana Kielimu**

- Kupiga vita ndoa za mapema.
- Kupiga marufuku ajira ya watoto.
- Wasichana wapewe nafasi ya kuendelea na masomo ya baada kujifungua.
- Alama za kujiunga na shule na vyuo vikuu kupunguzwe kwa wasichana.
- Elimu bila malipo kwa watoto wa shule za msingi na za upili.
- Kutoa msaada wa karo kwa familia maskini.
- Kujenga shule zaidi za wasichana.
- Mashirika yasiyo ya kiserikali kujenga shule na vyuo.
- Kuhamasisha wazazi kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto msichana.
- Adhabu kali kwa wabakaji. ***(Alama 20)***

**Swali La Pili:**

**a) Ufisadi Kama Kikwazo**

- Hii ni insha ya hoja.
- Hoja ziunge mkono kauli hii.
- Mtahiniwa akubaliane na kauli hii.
- Mtahiniwa ahusishe ufisadi unavyodumaza uchumi wa nchi.

**b) Hoja**

- Watu kupewa kazi wasizoweza.
- Wanaostahili kazi hawapati.
- Biashara haramu huwapunja raia.
- Wawekezaji huvunjwa moyo.
- Miradi ya maendeleo kukwama/kutomalizwa.
- Baadhi ya maeneo ya nchi kupuuzwa kimaendelepo.
- Nchi kukosa misaada.
- Taifa hutumia pesa nyingi kurekebisha ufisadi.
- Sifa za nchi kuharibika.
- uhalifu kuenea/kukosa usalama.

***(Alama 20)***

**Swali La Tatu**

**a) Methali: "Matikiti Na Matango Ndiyo Maponya Njaa"**

- Hii ni methali.

- Mtahiniwa atunge kisa/visa kuonyesha ukweli wa methali hii.
- Kisa kionyeshe sehemu mbili za methali.

  a) Upuuzaji/kudunisha kitu, jambo au mtu.
  b) Kitu, mtu au jambo hilo lije liwe ni la manufaa baadaye wakati wa shida.

**b) Msamiati wa methali**

- Matikiti na matango = aina ya vyakula visivyothaminiwa sana.
- Maponya = yanayookoa/yanayofaa
- Njaa = shida

**c) Maana ya methali**

Vitu tunavyodunisha/tunavyopuuza huweza kuwa na msaada mkubwa wakati wa shida. Kitu tulichonacho mkononi mwetu ndicho kinaweza kututoa taabani wakati wa shida, hivyo basi tusikidharau.

***(Alama 20)***

**Swali La Nne**

**a) Insha Ya Mdokezo**

- Hii ni Insha ya mdokezo na mdokezo huu ni wa kumalizia.
- Mtahiniwa atunge kisa kinachomalizikia kwa dondoo hili.
- Mtahiniwa ajihusishe katika kisa hiki.
- Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza
- Kisa kiwe na tendo/jambo baya kisiri
- Jambo hili linawekwa wazi
- Mhusika anakosa uso yaani anaaibika sana.

**b) Methali**: "Muungwana akivuliwa nguo huchutama".
**Maana**: Uovu wa mtu anayedhaminiwa ni mwema unapofishuliwa yeye huaibika.

***(Alama 20)***

## 30.2.2 Kiswahili Karatasi ya 2 (102/2)

**Swali la Kwanza**

(a)
- Uwanja wa sheria.
- Ushahidi waweza kutolewa mintarafu ya hisia zote. (tano)

***Au***

- Ushahidi huweza kutolewa mintarafu ya kuona, kusikia, kuguza, kuonja na kunusa.

***(Alama 3)***

(b)
- Hushindwa kukamilisha mwanadamu kuyafaidi maisha yake.
- Haimpeleki msomaji katika mipaka na nyanja za juu ufahanu na furaha.
- Msomaji hatapata mandhari kamili.

- Msomaji hataweza (atakosa) kushiriki katika matukio yenyewe.
- Fasihi itakuwa muflisi wa kisanii/fasihi itashindwa kuwasilisha mandhari ya hali halisi kwa msomaji.
- Hisia zisipotumiwa zote msomaji hataweza kutafakari zaidi.
- Msomaji hataweza kufikia uamuzi kuhusu picha zilizochorrwa.
- Huduma za sanaa.
- Hudhalilisha akili ya msomaji.
- Hataweza kuzama katika matendo na kuelewa fikra za mwandishi. ***(Alama 2)***

(c)

(i) Kazi nzuri ya sanaa ni ile inayohusisha hisia zote.(tano) ***(Alama 2)***

(ii)

- Humkamilisha mwanadamu ili ayafaidi maisha yake.
- Humpeleka msomaji katika miaka na nyanja za juu za ufahamu na furaha.
- Msomaji hupata mandhari kamili.
- Msomaji ataweza kushiriki katika matukio yenyewe.
- Huweza kuwasilisha mandhari za hali halisi kwa msomaji.
- Haitakuwa muflisi kisanii.
- Huweza kumfanya msomaji atafakari zaidi.
- Msomaji huweza kufikia uamuzi kuhusu picha zinazochorwa.
- Haitadumaza sanaa.
- Haitadhalilisha akili ya msomaji.
- Humwezesha msomaji kuzama katika matendo na kuelewa fikira za mwandishi.

***(Alama 4)***

(d) (i) ***Muflisi kisanii:***- Pungufu kisanii, hafifu, isiyoweza kutosheleza kisanii, duni, yenye kasoro au dosari, iliyo chapwa.

(ii) ***Jeraha la masaibu***:- Matatizo, machungu, mateso, taabu, shida, dhiki n.k.

(iii) ***Kumwashiki janabi***:- Kumhamasisha, kumteka, kumfanya apende, kumtamanisha, kumfanya avutiwe, kumteka akili, kumtia hamu au shauku.

(iv) ***Umbuji***:- Ubunifu, uundaji, ufundi, utunzi, ubingwa. ***(Alama 4)***

**Swali la Pili**

(a) Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo shughuli zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima ***kwa serikali*** huwa huria kwa ***watu binafsi***. ***(Alama 5)***

(b)

- Soko huru huwawezesha watu kuamua hatima yao kiuchumi.
- Suala ibuka ni kuweka mipaka baina ya shughuli zinazohusishwa na serikali na zinazoachwa huria kwa watu binafsi.
- Haki ya kuishi na kulinda dhidi ya shambulizi haiwezi kuachiwa watu binafsi.
- Huduma hizo zikiachwa huru zitaishia kuwa istihaki ya watu wa kipato cha juu.
- Huduma za kimsingi za afya haziwezi kubinafsishwa.
- Udhibiti wa kiserikali hutokea kuyalinda mazingira dhidi ya uchafuzi.
- Pia, udhibiti huo hutokea katika kulinda haki za watu binafsi. ***(Alama 10)***

**Swali la Tatu**

(a) Sahau ***(Alama 1)***

(b) Mfano wa sentensi yenye kivumishi cha nomino:

- Kijana mvulana amepita mtihani

AU

- Mtalii Mjerumani amewasili nchini. ***(Alama 1)***

(c) Wasichana watatu wanatoka / wanaondoka darasani polepole / ala ala / halahala / Aste aste / taratibu / kwa henezi. ***(Alama 2)***

(d)

(i) Ni kipashio kidogo zaidi cha lugha ambacho hakijaambishwa na kina maana ambayo imejisimamia / ni kamili. ***(Alama 1)***

(ii) ***Mifano:-*** Baba, mwalimu, kuku, simu, kalamu, kiti, sisi, chakula n.k. ***(Alama 1)***

(e)

- Kiambishi awali ni; -a
- Kiambishi tamati ni: -a au –ye AU –a na –ye ***(Alama 2)***

(f)

- Mwanafunzi yule ambaye ni mrefu amepita mtihani.
- Mwanafunzi yule ambaye amepita mtihani ni mrefu.
- Mwanafunzi ambaye amepita mtihani ni yule mrefu.
- Yule mwanafunzi ambaye amepita mtihani ni mrefu.
- Yule mwanafunzi ambaye ni mrefu amepita mtihani.
- Mwanafunzi yule ambaye ni mrefu ndiye amepita mtihani. ***(Alama 2)***

(g) Waya wangu umepotea. ***(Alama 1)***

(h) Yambwa tendwa / kipozi (shamirisho kipozi) ***(Alama 1)***

(i) Sentensi zizingatie maana zifuatazo za neno chuo:

- Ndoa – k.m. Zuhura hakuwahi kuolewa hata chuo kimoja.
- Kitabu kidogo cha dini / sala / maombi – k.m. chuo chake ndicho kilichomfaa sana wakati wa kutoa maombi hayo.
- Chombo cha kuchokolea nazi – Chuo cha mama kilipopotea, ilimbidi apike wali bila nazi.
- Mahali ambapo watoto hujifunza kurani / madrasa – k.m. Watoto wa dini ya kiislamu sharti wapitie katika chuo kujifunza kurani. ***(Alama 2)***

(j) Juzi, jana, Jumamosi, adhuhuri n.k. ***(Alama 1)***

(k)


- Alipiga mpira ***kumwelekezea*** Husha.
- Alipiga mpira kwa ***niaba ya*** Husha.
- Alimpiga kwa sababu ya kuuharibu mpira.
- Alipiga ili kumnufaisha / au kwa manufaa ya Husha.
- Alitumia mpira kama kifaa cha kumpiga Husha. ***(Alama 2)***

(l) Sisi hatujamaliza kujenga nyumba ambayo isingalikuwa yake asingalifurahi. ***(Alama 1)***

(m) (i) Zinguo, kuzingua, uzinguaji, uzinguzi, wazinguaji, mzinguliwa, wazinguliwa, mzinguzi. ***(Alama 1)***

(ii) Mtosaji / mtosi / mtoswa / kutosa / utosaji / mtoso / kitoswa / kitoso / utoso. ***(Alama 1)***

(n)



Paka mdogo amepanda mchungwani
*(Alama 4)*

(o) Mgeni yuko / yumo ndani ya nyumba. *(Alama 1)*

(p) Kusahili, sahili, sahilisha, sahilishwa, sahilika, sahilishiwa. *(Alama 1)*

(q) /z/ ni kikwamizo.
/d/ ni kipasuo. *(Alama 2)*

(r) Kitenzi kisaidizi *(Alama 1)*

(s) Kile / Hicho / Hiki *(Alama 1)*

(t)
- Sentensi sahili – Mfano: Mama anapika chakula. [Sentensi hii ina kitenzi kimoja na wazo moja]
- Sentensi ambatano – Mfano: Mtoto anacheza lakini mama anapika. [sentensi hii ina vitenzi viwili na mawazo mawili na pia ina kiunganishi] *(Alama 4)*

(u)
- Anasomea Ulaya.
- Aliwasili asubuhi.
- Amefika Dubai.
- Walitalikiana Mombasa. *(Alama 1)*

(v) Mvua imebomoa nyumba za majirani. *(Alama 1)*

(w) ***Kuakifisha***
"Huenda serikali iwazie kuidhibiti bei ya petroli.(;) H(h)atuwezi kuyaruhusu makampuni ya petroli kunyanyasa umma.(!)" Alisema Waziri wa Kawi. "Bei ya petroli imeongezwa mara nne katika kipindi cha mwezi mmoja!(.)" *(Alama 4)*

**Swali la Nne**

| SIFA | MFANO |
|---|---|
| 1. Kukatizana kalima | Mtu 1 – Kwa nini ulims……<br>Mtu 2 – Si mimi nilikwambia kwa ………<br>Mtu 1 – Ulimwambia nini? |
| 2. Kusitasita katika usemi | Baba - Eeem … nilisema eem … na ungeenda jana Nafikiri<br>Mama - … nadha..ni nitasafiri eem... pengine kesho |
| 3. Kutohoa | Ramadhani: Nimeshikwa na polisi afisini.<br>Juma : Hapana, ulishikwa katika stendi ya motokaa. |
| 4. Kuchanganya ndimi | Burhani : Julia alienda shopping before aende church to pray. |
| 5. Ishara | Chozano : Njoo hapa haraka (akimwonyesha anachotaka afanye kwa kuonyesha ishara kwa kidole cha pete)<br>Rukia : Nitakupiga, unaiitia nini? Akionyesha kwa mikunjo mingi usoni kuonyesha hasira) |
| 6. Uradidi –<br>(Kurudia usemi) | Mwoki : Hebu niambie ilivyokuwa.<br>Juma : Alienda, akaenda, akaenda…. |

| SIFA | MFANO |
|---|---|
| 7. Kukamilishiana usemi | Mtubora : Mtafika mape…<br>Mtusifa : Mtafika mapema.<br>Mtubora : Lakini msinichekele…<br>Mtusifa : Msinichekelee. |
| 8. Haizingatii sarufi sanifu - | Mtu mwenye aliniletea zile miti ndiye pia alinileteya kijiko yangu. |
| 9. Lugha ya kujibizana - | Mtu 1: Je ulienda nyumbani jana?<br>Mtu 2: Kwa nini unataka kujua?<br>Mtu 1: Ni kwa sababu kama hukwenda, ningependa kwenda nawe. |
| 10. Kuna usemi halisi | Juma : Je, ulimpikia chakula?<br>Sella : Ndio mama. |
| 11. Kuna wasemaji zaidi ya mmoja | Rashid : Twende home.<br>Okra : Sitaki.<br>Jura : Naelewa ni kwa nini hutaki kwenda huko. |
| 12. Mada hubadilikabadilika | Watu wawili au zaidi wanaweza kuanza mazungumzo yao kwa kulenga mambo ya siasa na wakabadili na kuzungumza mambo ya dini au hata mambo yanayohusu kilimo. |
| 13. Kuna kugeuza ndimi | Mtu 1: Come quickly. Si vyema unavyofanya. Why don't you consider the repercussions. Fikiri vema tena.<br>Mtu 2: Ahaa, wewe ndiye unajua vema? Why do you interfere with my plans? Usiingilie mambo yasiyo kuhusu. |
| 14. Ucheshi na utani | Sundo : Aya!Umekula ugali kama mlima?<br>Pasua : Nenda mbali na matungamavi yako!<br>Sundo : Je, mbona unapunguza hicho chakula ilhali mdomo wako ni mkubwa? |
| 15. Kuna matumizi ya tamathali za usemi | Wasemaji wanaweza kutumia chuku, nidaa, tashtiti na hata kinaya wanapozungumza<br>***(Alama 10)*** |

**30.2.3 Kiswahili Karatasi ya 3 (102/3)**

**Swali la Kwanza**

(a)
- Wanajamii wanajishughulisha katika kazi mbalimbali ili kuboresha maisha yao lakini maisha yao ni duni.
- Vibarua wanaoajiriwa wanafanya kazi kwa bidii lakini mishahara yao ni duni.
- Viongozi serikalini wamepewa nyadhifa hizo za hadhi lakini hawawajibiki kwa wale waliowachagua, hawawajibiki kunyanyua hali za wale waliowachagua.
- Tabaka la chini ndio walio wengi katika jamii na ndio tegemeo la jamii lakini wanaishi maisha ya mateso mengi.
- Haijulikani mateso ya walio wengi yatafikia kikomo lini. ***(Alama 4)***

(b) (i) **Kinaya**
- Wasakatonge ndio wengi lakini hawana sauti.
- Makuli, mayaya, manamba, wachapakazi, madobi na matopasi ni maskini
- Wasakatonge wafanyao kazi kwa mateso mengi ni wenye mishahara duni.

- Wapelekao watu serikalini hawashughulikiwi na waliowachagua.
- Wazalishao mali hawana chochote bado maskini.

(ii) **Taswira**

- Wabeba zege maroshani
- Msukuma mikokoteni
- Makuli bandarini
- Manamba mashambani
- Wachapakazi viwandani
- Matopasi wa majaani
- Wanasiasa madarakani
- Mayaya na madobi wa nyumbani siku zote wako matesoni.

(iii) **Takriri**

- Wasakatonye
- Juakali
- Lakini limetumiwa mwanzoni mwa kila mshororo wa mwisho wa ubeti (kikwamba)
- Wao
- Ni

(iv) **Ulinganushi**

- Wachimbaji wa migodi lakini maisha yao chini
- Wachapakazi viwandani lakini bado ni maskini. ***(Alama 3)***

(c)

- Kipande kimoja
- Shairi lina kituo, kimalizio
- Mizani hailingani katika kila ubeti
- Beti 4
- Mishororo 6 kwa kila ubeti (Tasdisa, usita) au kila ubeti una kishwa/kijichwa, anwani na mishororo 5.
- Katika mshororo wa kwanza vina vinabadilika – LI na NGE
- Mishororo mitano ya mwisho ina vina vinavyofanana – NI
- Pindu – mshororo wa kwanza unajipindapinda. ***(Alama 5)***

(d) Watu wa tabaka la chini ndio huwapa nyadhifa viongozi. Kutokana na nyadhifa hizo viongozi hupata mali au uwezo wa kiuchumi (kuiongoza nchi). Wale waliowachagua maisha yao ni ya kusikitisha. ***(Alama 4)***

(e)

- Kufanya kazi kwa bidii
- Kuwajibika – kwa umma katika kushiriki katika kuwachagua viongozi
- Viongozi wanatarajiwa kuadilika kwa kunyanyua hali ya umma kwa kujali hali ya wafanyakazi. ***(Alama 2)***

(f)

- Manamba – Vibarua/wafanyikazi katika mashamba
- Tabaka lisilo ahueni - watu maskini/wasio na hali nzuri kiuchumi/walalahoi

***(Alama 2)***

**Swali la Pili**

(a)

- Maelezo ya sauti kuhusu uwezo mkubwa wa jua ambao Mtemi Bokono hawezi kunyanyasa au kutesa. Uwezo wa jua unaashiria uwezo wa umma ambao utamwangamiza Bokono. Bokono amekuwa na uwezo wa kufanya mambo mengi lakini uwezo wa jua unaashiria kwamba umma una uwezo utakaomzidi Bokono na kumng’oa mamlakani.

- Kutokuwepo watu katika mkutano wa Mtemi Bokomo ni dalili kwamba watamwasi hatimaye. Watu hawakuwa na imani na uongozi wa Bokono kwani walikuwa wamechoshwa nao.
- Ndoto ya Mtemi Bokono kuhusu kuzikwa kwake kaburini akiwa hai ni ishara ya kuangamizwa na kuzikwa kwa utawala wake. Ndoto inaonyesha dalili ya kwamba ingawa Bokono angali hai, wanabutangi hawamtaki tena hivyo basi anazikwa angali hai, yaani kutolewa mamlakani akiwa bado ni kiongozi.
- Tendo lake la kushika mkia wa Mjusi/nyoka anayemuuma na kumwachia sumu ni ishara ya matokeo na hatari ya kuchezea haki za wananchi. Bokono kupuuza upinzani wa wanabutangi kwani hawaamini uongozi wake una hitilafu.
- Ndoto ya Tanya kuhusu simba mkubwa aliyelala kando ya kisima ni ishara ya kiongozi anayewazuia watu kufaidi rasilmali ya umma na uhuru. Uongozi wa Bokono umehodhi mali na kuwazuia wanabutangi uhuru wa kufaidika nayo.
- Ndoto ya pili ya Tanya kuhusu kichwa cha simba kinachobadilika badilika kuwa na sura ya Mwelusi ni mdokezo wa ishara ya Mwelusi anayeuawa na nduguye Gege.
- Masimulizi ya Askari 1 kuhusu kisa cha jirani aliyelewa hoi na kuwa nusu maiti huku akichekelewa na jua ni ishara ya kiongozi anayepagawa au kulewa mamlaka anavyofanya Mtemi Bokono. Hatima ya uhai (maiti ya mjusi) inaashiria kikomo cha uongozi wa Bokono
- Nyalwe kutoa picha ya Bokono kurudi tumboni ni kuashiria kuisha au kusahaulika kwa uongozi wa Bokono.

***(Alama 20)***

**Swali la Tatu**

(a)
- Katika kisima cha Mkomani – Bonde la Ilangi
- Msemaji ni Zigu mmojawapo wa washauri wa Mtemi.
- Anazungumza na Kaloo
- Kaloo angependa kutoa shukurani kwa Mtemi kwa sababu Mtemi aliamuru mtoto wake apewe kazi/Kaloo kutaka kumshukuru Zigu kwa kuzungumza na Mtemi. ***(Alama 4)***

(b)
- Ni watu wa kuitikia kila kitu anachosema Mteni Bokono.
- Wanamlimbikizia kiongozi wao sifa zisizo za kweli kama vile mtukufu, Baba wa Butangi, Mtukufu wa Busara, Kiongozi mwema, mzazi bora kuliko wengine na kadhalika. Sivyo kwani watu walinyimwa maji kisimani, uwanja wa watoto ulinyakuliwa na kadhalika.
- Wanadai Mungu amempa Bokono utawala. Angetawala kwa haki bila malalamiko.
- Wanamhimiza kuongoza Butangi kwa miaka 100. Haiwezekani.
- Wanamsifu Bokono kwa kuongoza kwa busara kwa manufaa ya wote mf. Waliofaidika ni wachache wa aila yake.
- Wanadai Bokono anapendwa na wote na si kweli. Watu walisusia mkutano. Nyalwe kumwambia hapendwi.
- Wanamsifu Bokono kwa uvumilivu wake. Mf Vitisho vya kutafuna mifupa/majibu ya kuondoa mwiba.
- Wanakumbusha ushauri wa Bokono kuwa watu waishi kwa upendo na amani ingawa si kweli. Mf. Vita vya wenyewe kwa wenyewe.
- Hawamwambii ukweli na hali ilivyo mf. Mkutano unaposusiwa wanamhimiza kwamba watu watakuja tu. Licha ya Kame kuwa mshauri wake anafanya mambo ambayo ni kinyume cha utawala wa Bokono.
- Wanaompinga wananyimwa nafasi ya kuchota maji kisimani na ilhali ni mengi. ***(Alama 16)***

**Swali la Nne**

**Mwisho wa Kosa**

- Wanawake hasa wazee hawakujua kusoma au kuandika. Bi Tatu anatafuta mtu wa kumsomea barua.
- Wanawake wanajihusisha tu na biashara ndogo ndogo kama za uji na sukuma. Wafanyabiashara maarufu kama Selele ni wanaume
- Wanawake wanakumbwa na umaskini. Mfano Bi. Keti mwanzoni mwa riwaya
- Wanawake walihimizwa kufanya kazi fulani kama kusomesha. Km Saidi babake Muna alimshawishi hadi akakubali ualimu.
- Wanaume ndio walioamua masuala kuhusu posa. Jambo hili tunaona likitekelezwa na Saidi, Salimu na babake Ali (Selele).
- Wanawake waliwazia ndoa tu hasa baada ya kuvunja ungo. Zahara, mtoto wa miaka 16 anawaziwa Posa.

- Mwanamume alikuwa na hadhi kuu nyumbani "… ndiye mkuu wa nyumba, anayelisha na kuvaza nayojua yale yanayopita nje katika ulimwengu…" (uk.127)
- Udhibiti wa wanaume kwa wake zao. Waliamua shughuli wanazoshiriki, namna wanavyovaa, n.k. Salimu anasisitiza: "Hasani ana haki kutenda analotaka kwake, na kumwamrisha mkewe" (Hasani alivyomdhibiti Muna).
- Mwanamke alitarajiwa kuficha uhodari na ufanisi wake. Muna na kazi yake.
- Masuala kuhusu watoto/wanafunzi wa vyuo vikuu yanashughulikiwa na wanaume. (Bushiri alivyoitwa chuo kikuu kumhusu mwanawe Ali).
- Wanaume walikuwa na uhuru wa kuingiliana na watu wengi bila jamii kuwashuku lakini kwa wanawake jambo hili halikuruhusiwa.
- Katika jamii nzima hatuoni mwanamke aliye na cheo. Hata Monika aliye na masomo ya chuo kikuu hawezi kupewa cheo, hana gari anabaki kumtegemea Rashid.
- Monika anabaki kuozwa kwa mtu asiyekuwa na elimu ya juu kwa lazima kama adhabu/sharti la kukubalika tena katika jamii yake na familia.
- Licha ya mali na nafasi aliyokuwa nayo, Bi. Maryamu hatumwoni akichangia katika maendeleo ya jamii yake.
- Asha kupewa nafasi inayoendeleza uongo na uharibifu mf. Mumewe kucheza kamari naye kumzingizia wizi Bi. Keti.
- Salama ni msomi na mfanyakazi ilhali hakui kama mhusika, anakaa akimsubiri Rashid amwoe.
- Katika maswala ya sheria wanawake wamechorwa kama wasioweza kujitetea. Ilibidi Haji aingilie kati kuhakikisha Keti ameachiliwa naye inspekta Hamisi alimsaidia Bi. Maryam.
- Ingawa Monika ana kazi na mshahara mkubwa hachangii maendeleo k.m. hawasaidii wazazi, nduguze na jamii/anafuja pesa zake. ***(Alama 20)***

**Swali la Tano**

(a) **Makosa ya Ali**

- Tangu utotoni mwanzoni alikuwa mgomvi na kulikuwa na matatizo mengi baina yake na walimu.
- Alizozana na watoto wa majirani pale nyumbani.
- Alipoingia chuo kikuu alijishughulisha sana na mambo mengine kama siasa chuoni.
- Alipenda anasa na alikuwa na marafiki wengi wa kike kinyume na matarajio ya jamii.
- Ingawa alikuwa hodari mahudhurio yake kwenye mihadhara hayakuwa mazuri na mtihani ulipofika alijipata hajajiandaa/hajadurusu.
- Alikubali ushawishi wa kutumia dawa za kulevya kinyume na sheria za chuo.
- Ali daima hakuzingatia nasaha ya wasimamizi wa chuo na akakataa kurekebika
- Wasimamizi wa chuo walimwita babake azungumze na Ali na pia hakubadilika.
- Alikataa kukiri na kufichua aliyemuuzia vidonge. ***(Alama 8)***

**Mwisho wa Kosa**

Anapofukuzwa chuo kikuu alijisaka nafsi yake na kujirekebisha. ***(Alama 2)***

(b) **Makosa ya Asha**

- Asha alimwonea wivu Keti. Mf. Wenzake walipomfurahia Keti katika harusi yake, yeye alifanya kinyongo.
- Asha alimchukia Keti kwa uzuri wake.
- Alikuwa mwanamke mwenye kiburi – hakuwa mtiifu. Alipotumwa na mamake kuleta kibweta alinuna na alipoashiriwa kutoka ili mamake aseme na Keti faraghani alisita.
- Alibadilisha vyombo vya dhahabu alivyoazima Bi. Keti na kurudisha vile vya thamani ya chini.
- Asha alimzingizia Keti, jambo lililofanya kufunguliwa mashtaka.
- Alikuwa mwongo – alikuja kukaa kwa mamake kwa kusingizia ugomvi na mumewe kumbe walikuwa wamepanga kuiba vyombo vya dhahabu.
- Asha aliiba vyombo vya dhahabu alivyorudisha Keti.
- Tabia ya kuiba, kukopa na kuweka rehani vitu ili kumpa mumewe mcheza kamari.
- Asha hakufurahia makubaliano baina ya mamake, Bi Mariyamu na Keti ya kulipa vyombo vya dhahabu pole pole (alikuwa katili kwa kutaka Keti aumie).
- Kuficha tabia mbovu za mumewe hasa uraibu na kucheza kamari. ***(Alama 8)***

**Mwisho wa Kosa**

Makosa haya yote yanabainika inapofichuliwa mbele ya ndugu zake na inspekta kuwa Asha alikiri kwa mamake Bi Mariyamu kuwa ndiye aliyechukua vyombo vya dhahabu. ***(Alama 2)***

**Swali la Sita**

**"Umdhaniaye Ndiye, Kumbe Siye."**

Kwa kurejelea hadithi tano kutoka kwa diwani ya ***Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine***, onyesha ukweli wa methali hii.

**Majibu**

**(a) Pwaguzi**

- Shehe Kijuba katika hadithi pwaguzi pamoia na waumini wengine walikuwa wamemwamini Salimu kuwa ni mwalimu mzuri wa dini. Wakazidisha imani yao kwake walipoingia katika mpango wake wa ulaghai wa kibiashara. Wakampa pesa nyingi ili wafanye biashara ya kuuza viazi. Ukweli ulipowabainikia, waliyemdhania kuwa mwalimu mzuri wa dini na msalihina kumbe lilikuwa pwaguzi.
- Shehe kijuba kujifanya shehe na kuaminiwa na watu. Alipokea pesa za sadaka na chai na kuzitumia kwa manufaa yake. Imani waliyokuwa nayo waumini kwake hawakudhani angewatendea hivyo.

(b) **Fumbo la Mwana**

Mzee Atanasi na familia yake katika hadithi Fumbo la Mwana, walimwamini Makulu jirani kuwa mtu mzuri na mfanyibiashara mkarimu. Watu wengi kitongojini nao pia walimwamini na walienda kununua kutoka duka lake. Imani ya Atenasi kwa Makulu ilimfanya amtoe mwanawe Nanda awe akimsaidia Makulu. Wakati hulka za Nanda zinapoanza kudhoofika, imani ya Atanasi kwa Makulu haimwelekezi kushuku rafiki yake. Baadaye Atanasi anapigwa na butwaa kuona kuwa mharibifu wa mwanawe ni yule aliyemwamini sana. Kweli umdhaniaye siye, kumbe ndiye.

(c) **Msamaria Mwema**

Wahudumu hospitalini, katika hadithi ya Msamaria Mwema waliamini kuwa mtu aliyempeleka Likono hospitalini ni msamaria mwema. Alijitetea kuwa yeye ni msamaria mwema aliyempata Likono kama amegongwa na gari. Kumbe, sivyo, yeye ndiye aliyemgonga kwa gari lake.

(d) **Siku ya Mganga**

Wagonjwa katika hadithi ya Siku ya Mganga walimwamini Mwaibale sana kuwa ni mganga hodari mwenye uwezo wa kutibu kila aina ya maradhi. Walimpelekea nyembe ambazo walimtaka awe akizitumia kumchanja kila mgonjwa na wembe wake. Waliamini Mwaibale aliyaelewa haya. Kumbe hakujua sababu yake. Mwaibale aliendelea kutumia wembe mmoja kwa kila mgonjwa huku akiwahadaa kuwa alikuwa anatumia wembe tofauti kwa kila mgonjwa. Kupitia kwa wembe huo, wagonjwa wengi waliathirika na kupata ukimwi. Hata mganga hakuponyoka kweli.

(e) **Uteuzi wa Moyoni**

- Mzee Said, Babake Zena katika hadithi ya uteuzi wa moyoni aliamini kuwa mume aliyetokeza kumwoa Zena ni nzuri na kuwa angemtunza bintiye na maisha mema ya ndoa. Haya hayakutimia. Kwani Ali alikuwa nduli, mlevi, aliyempiga bintiye hadi Zena akadai apewe talaka. Mzee anaomba msamaha kwa bintiye kutokana na imani yake potovu. Umdhaniye ndiye, siye.
- Uchaguzi wa mbunge mwanamume aliyedhaniwa angewasaidia wananchi, aliishia kutokomea mjini na kuwasahau, kinyume na jinsi walivyotarajia atimize kazi yake ya ubunge.

(f) **Ngome ya Nafsi**

Kuozwa kwa Naseko, alifikiriwa kuwa ameshafikishwa kwa boma la mumewe. Vijana waliombeba walikuwa wamekamilisha jukumu lao, naye Sakaja kuona ameshaletewa mke. Hatimaye Naseko anatorokea kwa Bi. Tesi na hivyo basi aliyedhaniwa ni mke wa mzee Sakaja, siye.

(g) **Kachukua Hatua Nyingine**

- Bintiye Mavitu kupewa mimba na jirani aliyekuwa amemwajiri, ambaye alikuwa ni mtu mzima aliyetarajiwa kumtunza.
- Mfadhili aliyemsaidia Mavitu kwa fedha lakini hatimaye alikuja kumega kipande cha shamba la Mavitu. Ilikuwa mbinu tu ya kumwibia Mavitu kipande cha shamba.

(h) **Tuzo**

Kibwana alimwamini Salome alipomwambia ndiye mshindi wa Tuzo. Kibwana alijitayarisha vilivyo kwa siku hiyo lakini aliyepata tuzo mwishowe alikuwa Salome.

(i) **Mayai**

Waziri wa Maradhi aliomba maradhi ya kipindupindu yaongezeke ili idadi ya watu ipungue. Mayai alimpenda mwanawe Ukombozi sana lakini Ukombozi anaporejea kama mzuka, anawakashifu viongozi kama babake Mayai.

(j) **Mkimbizi**

Vita vya kikabila vilipozuka kati ya wahutu na watutsi, haikuaminika kwani watu hawa walikuwa wameishi pamoja kama majirani na ndugu lakini walikuja kugeukiana na hata kuuana.

***(Alama 20)***

**Swali la Saba**

- Matumizi ya ucheshi
- Kuielewa hadhira – kutambua hadhira yake na kutambua ni ngano ipi inayofaa/mada ipi/mbinu zipi muhimu.
- Matumizi ya ishara za mikono na uso kuukuza na kuendeleza ujumbe (mazaja)
- Uteuzi wa lugha unaofaa – sajili, msamiati
- Ushirikishaji wa hadhira yake.
- Kuibadilisha toni/sauti yake kutegemea ngano/visa/au wahusika.
- Ufaraguzi kuweza kuibadilisha ngano au kuifanyia mageuzi kutegemea hadhira/kuweza kuipa ngano upya fulani.
- Kuielewa jamii yake – mambo yanayoathiri katika shughuli za kila siku.
- kuielewa desturi ya jamii yake/kuelewa sifa za utamaduni wenyewe.
- Ufahamu wa kina wa lugha/kuweza kuyaeleza maneno ambayo jamii haiyajui (ukwasi)
- Uwezo wa uigaji – kama ndege, fisi.
- Kuteua mbinu za kuwasilisha mf. Nyimbo, tamathali za usemi.
- Ubunifu wa hali ya juu.
- Kumbukumbu nzuri
- Ukakamavu/ujasiri
- Mtambaje awe na uwezo wa kusikika na hadhira yake/kupasa sauti. ***(Alama 20)***